**LBE KOMPUTA NA MTANDAO WA INTANETI –KIPINDI CHA KWANZA**

**Mwandishi :** Richard Lough

**Muhariri:** Thomas Mösch / Katrin Ogunsade

**Tafsirib : Eric Ponda**

**Wahusika :** Beatrice (msichana wa makamul), John (Mvulana wa makamu), Sauti ya Komputa)

Sauti : Peter Wakasiyaka (Menja wa kituo cha Komputa), Doris miaka 19, mwanafunzi wa somo la Komputa.)

**Sauti ya Msimulizi:**

*Muziki – [sekunde 0:10 na kutowekwa chini kwa chini.]*

**Intro:**

Hujambo na karibu kwa mfululizo wa vipindi vyetu vya Noa Bongo Jenga Maisha yako kuhusu mitambo ya Komputa na Intaneti. Katika kipindi cha leo, John na Beatrice wanapata elimu ya kimsingi kuhusu matumizi ya Komputa. Ndio mwanzo kabisa kujifunza matumizi ya Komputa na hatimaye mwishoni mwa kipindi bila shaka hata wewe pia utakuwa umejifunza mengi, kama vile jinsi ya kufungua na kuzihifadhi faili zako kwenye Komputa.

Pia tutakuonyesha jinsi ya kucheza kanda za ***CD*** na ***VCD*** kwenye komputa yako.

**Package 1.1**

**SFX_*Komputa inafunguliwa*.**

**1. Komputa**: Karibu John na Beatrice kwa ulimwengu wa Komputa. mukiwa tayari, munaweza kubonyeza, alama ya ***Return Key*** kwenye ubao wa Komputa yenu .

**2.John:** Oooh Beatrice Komputa inaongea! Tazama Beatrice, kuna alama hiyo upande wa kulia wa ubao wa komputa.

**SFX_Sauti kubonyeza alama**

**3.Komputa :** Vyema!. Sasa ukinitizama unaweza kuniambia ni vipi vijenzi vitatu ,***yaani Komponeti tatu***

**4.Beatrice:** Skrini au kio cha komputa…

**SFX…_*Ping.. [ kama ile suati unayoisikia kwenye mchezo unapopata jibu sahihi.]***

**5. Komputa:** Umepata. Nini tena …?

**6.John:** Ubao wa Komputa….

**SFX_*Ping[ kama ile suati unayoisikia kwenye mchezo unapopata jibu sahihi.]***

**7. Komputae:** Umepata!. Na nini tena…?

**8.John/Beatrice:** Ummm…

**9. Komputae:** ***Hard-drive***. Hili kidogo ni gumu.Lakini usijali kuhusu hilo kwa sasa!.

**SFX_ *Ukurasa wa Komputa-Windows_ unafunguka***

**10. Komputa:** Mimi hutumia mfumo wa teknolojia ujulikanao kama ***Microsoft Windows..***

**11. Beatrice:** Kuna mifumo mingine?

**12 Komputa:** Ndio, iko mifumo mingine. Kuna mifumo kama vile ***MAC OSX*** na ***Linux*** lakini tusijali kusuhu majina hayo Kwa sasa,unachopasa kujua, ni jinsi ya kutumia komputa. Sasa skrini au kioo cha komouta unachokitizama sasa hivi inajulikana kama ***Desktop***. Skrini hii ndiyo muongozo wa programu zote kwenye komputa. …

**13. Beatrice:** Hii ni kumaanisha nini?

14 **Komputa:** Katika Skrini hii, utakuta kila ukurasa wa tovuti au huduma unazotaka kutumia kwenye komputa. Sitamueleza zaidi kwa sasa lakini tutajifunza jinsi zinavyotumika katika makala yetu ya hapo baadaye. Sasa bonyeza alama ya ***Start*** katika ubao wa Komputa ili kufungua komputa hiyo…

**SFX_ *Sauti ya kibonyezo***

**15. John:** Sawa!.

**16. Komputa:** Kisha bonyeza alama inayooneyesha Programu zote ***`yaani All Programmes’*** kwenye skrini ya ya komputa yenu

**SFX_ Sauti:Anabonyeza mara moja**

**17. Beatrice:** Tayari. Ooh … Kwa hiyo una programu zote hizi?

**18. Komputa:** Ndio.

**19. John:** Unaweza kufungua Programu nyingine kwa wakati mmoja?

**SFX_ *Sauti: Bonyeza mara mbili ...mara tatu***

**20. Komputa:** Ndio. Nimekufungulia programu nyingine tatu. Moja ya Intaneti, nyingine ya kuandikia. yaani ***`Word´*** na nyingine ya kucheza kanda ya ***CD***

**21. Beatrice:** Na hebu John tazama chini ya Skrini hii, kunavijisanduku…

**22. Komputa:** Ni kweli, Beatrice. Vijisanduku hivi vinakuwezesha wewe kutoka Programu moja hadi nyingine kwa kubonyeza ***Mouse***

**23. John:** Sasa ni vipi Mtu anaweze kuhifadhi kazi zake kwenye Komputa? Kwa mfano unapoandika insha shuleni.

**24. Komputa:** Ni lazima uhifadhi kila faili unayofungua iwapo unatakakuendelea kuitumia. Kwa hivyo unapotumia faili hii ya ***Document***, unaweza kubonyeza alama ya ***`File´*** upande wa kushoto juu ya skrini yako, na kisha kubonyeza alama ya kuhifadhi yaani ***`Save´*** kuhifadhi kazi yako

***SFX_Bonyeza mara mbili***

**25. Komputa:** Vyema ,inasema nini?

**26. Beatrice:** Inataka jina la faili yako na mahala unapotaka kuihifadhi faili hiyo.?

**27. John:** Utajuaje jina la faili yenyewe?

**28. Komouta:** Unaweza kuipa jina lolote tu. Lakini sio jina ambalo tayari umelitumia kwa faili nyingine ulizozihifadhi kwenye komputa, la sivyo utazifuta faili za awali.

**SFX_** ***Akiandika jina la faili***

**29. Beatrice:** Na sasa utazihifadhi wapi faili zote hizi?

**30. Komputa:** Ah! Unaweza kuchagua ***[SFX_Komputa ikiunganisha mawasiliano.]*** Kila komputa inakifaa au sehemu ijulikanayo kama ***Hard Disk*** au ***Hard Drive***. Hii ni kama hifadhi au ghala. Idadi ya faili unazotaka kuzihifadhi kwenye komputa yako,hutegemea ukubwa wa kifaa hiki cha ***Hard Drive***.

**31. John:** Na je, nitaipata vipi faili,iwapo nataka kuitumia tena ?

**2. Komputa:** Pia kuna kifaa kidogo unachoweza kubeba faili kutoka kwa Komputa, pia hii ni kama hifadhi inayojulikana kama ***Flash Drives*****.** Kifaa hiki ni kidogo kuliko zile ***Drives*** zinazopatikana kwenye komputa,na ni rahisi kukibeba wakati wowote mahali popote..

Kifaa hiki unaweza kukitumia katika komputa nyingine kupata faili zako.

**33. John** ***(anatokwa na subra):*** Na nikitaka kutazama filamu kutoka kwa ***DVD?***

**34. Komputa:** Siku hizi, komputa nyingi zimetengenezwa na sehemu au huduma za kucheza ***CD*** na ***DVD.*** Hebu niangalie vizuri, utapata niko na moja kasha uifungue.

**35. Beatrice:** Ndio hii hapa.

**SFX_CD_** ***inajifungua***

**36 Komputa:** Sasa weka ***CD*** au ***DVD*** kama vile tu unavyoweza kuweka kwenye redio yako kisha funga.

**SFX_CD_ *Inajifunga***

**37. Komputa:** Kisha rudi kwenye skrini yako na ufungue ukurasa wa programu utaona sehemu imeandika ***Audio au DVD***,bonyeza alama hiyo kama itakuwa haijajifungua.

**38. John:** Subiri…

**SFX_*Anabonyeza mara mbili…***

**39. John:** Bonyeza ***Play*** au Cheza…..

**SFX_*Muziki [mchanganyiko wa nyimbo] sauti inatoweka chini kwa chini***

**40. Komputa:** Kumbuka pia unaweza kuhifadhi faili zilizoko kwenye ***CD*** au kunasa Muziki huu kwa kanda nyingine ya ***CD*** na ***DVD*** ambayo haijatumika. Eendelea kufurahia ….

**Muziki**

**Music – Full up for 0:10 then fade under Intro_Part_B**

**SFX_Gordon_Teaching_3 [Full up 0:10 then fade under]**

**1. Beatrice:** Hii ni taasisi inayotoa mafunzo ya juu ya Teknolojia ya mawasiliano ya Komputa Jijini Nairobi nchini Kenya.

Nimekuja hapa kwa kozi ya Teknolojia ya mawasiliano inatolewa kwa wanafunzi ambao ndio mwanzo wanajiunga na mafunzo hayo kama mimi. Katika darasa hili Gordon ni mkufunzi wa wanafunzi saba ambao sasa wanajifunza Programu ya ***Microsoft Windows*** inayojulikana kama ***Excel…***

**SFX_Gordon_Teaching_3 [Full up again for 0:05 then fade under next track]**

**2 Beatrice:** Anayenieleza kuhusu kozi zinazotolewa katika taasisi hii ni meneja wa taasisi hii Pater Wakasiya.

**X-ade into SFX_ Darsa la Ambie**

**Clip: 1.2_Wakasiyaka_1**

Hapa tuna Kozi zinazofahamika sana kama end-user: Hizi ni Kozi zinazomuwezesha mwanafunzi kujua jinsi ya kutumia Komputa, ingawa neno hili la ***End-user*** san asana hutumika katika programu za ***Microsoft Office*** kama vile ***Powerpoint, Word, Access na Excel*** ambazo ni hutolewa kwa wanafunzi wanaoanza kujifunza Komputa

**3. Beatrice:** Zaonekana Programu nzuri zinazowafaa wanafunzi wapya kama mimi anayehitaji mafunzo ya kimsingi, kama vile kuandika insha, na jinsi ya kufungua kurasa nyingi kwenye skrini ya komputa yako na kadhalika. Je unawanafunzi wengi kama mimi.?

**Clip: 1.2_Wakasiyaka_2**

Wengi wanaojiunga na chuo hiki huwa na watu ambao hawajui chochote kuhusu Komputa na huwa wanataka elimu ya kimsingi kuhusu matumizi ya Komputa, kwani wanafunzi wengi wanaojiunga na vyuo kwa mfano chuo kikuu wanalazimika kufanya kazi zao kwa

**SFX_Gordon_Teaching_2 [Full up then fade under track]**

**4. Beatrice:** Sasa wanafunzi wanaonyeshwa jinsi ya kuchora grafu kutoka kwa Data kwa ripoti ya utafiti. Nataka kujua ni sababu ya wanafunzi hawa kujiunga na darasa hili.…

**Full up SFX_Gordon_Teaching_2 then X-fade into SFX_Ambie_Classroom**

**Clip: 1.2_Doris_1**

Nataka kufanya taaluma ya uhasibu. Nataka kuwa mhasibu. Na hii ndiyo sababu najijifunza Komputa ili niweze kufanya kazi zangu kwa makini zaidi..

**5. Beatrice:** Vyuo vingi jijini Nairobi na hata kote nchini Kenya ni sharti Mtu awe na ujuzi wa kutumia Komputa. Kabla ya kuanza kozi ya wiki 13, Doris mwenye umri wa miaka 19, anakiri kwamba hakuwa akijua lolote kuhusu Komputa kama mimi.

**Clip: 1.2_Doris_2**

Nilikuwa nikiona Komputa kama kioo tu, na nilidhani ni chombo cha kupiga chapa. Sikujua jinsi ya kuitumia . Lakini baada ya kupata mafunzo sasa naweza kuitumia vizuri..

**Add SFX_ *akipiga chapa taratibu kwa kutumia komputa.***

**6. Beatrice:** Nitaka kumuuliza Peter Wakasiyaka iwapo kuna njia nyingine Mtu anaweza kujifunza kutumia Komputa. Kwa Mfano iwapo siko karibu na chuo cha mafunzo ya Komputa.

**Fade out SFX_akipiga chapa taratibu kwa komputa.**

**[Keep SFX_Ambie_Classroom as bed]**

**Clip: 1.2_Wakasiyaka_4**

Kuna mitandao mingi tu hasa kwa wale wenye ujuzi wa kutumia mtandao wa Intaneti, ikifungua ukurasa wa ***Google*** ambao haona malipo yoyote, unaweza kujifunza kutoka mwanzo. Ila changamoto zilizopo,ni kwamba ni vigumu kidogo kwa Mtu ambaye si mwepesi wa kufanya utafiti. Au kuelewa vizuri masuala ya Intaneti.

**7. Beatrice:** Kwa hiyo mafunzo ya kupitia mtandao wa Intaneti ni mazuri kwa kuwa unaweza kuyakamilisha kwa wakati wako upendao, Au kuchagua kozi ambayo haina malipo yoyote? Lakini inaonekana kwanza ni lazima umwe unaelewa jinsi ya kutumia komputa. Na kama,kozi hizi hizipendi je kuna njia nyingine ya kujifunza kutumia Komputa- kwa mfano kumuuliza Mtu akusaidie Peter?

**Clip: 1.2_Wakasiyaka_5**

Ndio unaweza , kama wewe ndio mwanzo unajifunza Komputa , itakuwa vigumu kidogo kufungua programu za mitandao ya Intaneti..

**8. Beatrice:** Hapana shaka, kwamba si kila Mtu anaweza kupata huduma za Intaneti. Wengi hawajaunganishwa au kubahatika kuwishi

karibu na kumbi zinazotoa huduma hizo, na hata kama pengine ziko, ni ghali mno! Je kuna vitabu vya watu wanaoanza kujifunza Komputa?

**Clip: 1.2_Wakasiyaka_6**

Ndio viko vitabu . Ikutembea barabara za Nairobi utavikuta. Vitabu kuu vikuuzwa. Vinaitwa ***Dummies***…Vitabu hivi vya ***Dummies*** vinaweza kumuelekeza Mtu… Na ni vingi kila mahali, vimerahisishwa ili kumsaidia Mtu anayeanza kujifunza Komputa.

**9. Beatrice:** Lakini mimi binafsi ningependa kufunzwa na Mwalimu ili aweze kunisaidia wakati wowote.

**Outro:**

Ni hayo tu tuliyoweza kukuandalia katika kipindi cha leo kuhusu mafunzo ya Komputa na Intaneti. Katika mfululizo wa vipindi hivi utajifunza mengi kuhusu mada zilizozungumziwa katika kipindi hiki. Kumbuka ukitaka kukisikiliza tena kipindi hiki au labda pamoja na rafiki zako unaweza kutembelea tovuti yetu: www.dw-world.de/lbe.
Hadi wakati mwengine Kwaheri.